# RIPOTI YA HIARI YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU (SDGs)

## Tanzania imesifiwa kwa kutekeleza vyema Sekta ya Elimu Uk.2



# RIPOTI YA HIARI YA UTEKELEZAJI WA SDGs

## Tanzania imesifiwa kwa kutekeleza vyema sekta ya Elimu




Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango akiwasilisha Ripoti ya Hiari ya Tanzania huko New York Mjini Marekani, 2019

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ziliandaa ripoti ya pamoja ya hiari (VRN) kuhusu utekelezaji wa Malengo sita (6) kati ya 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa na kuyawasilisha kwenye Mkutano wa Jukwaa la Kisiasa la Ngazi za Juu (High Level Political Forum – HLPF) uliofanyika Mjini New York, nchini Marekani.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Zanzibar imejipatia sifa kubwa kutokana na ripoti yake ya hiari VRN iliyowasilishwa kwenye Mkutano wa Jukwaa la Kisiasa la Ngazi za Juu (High Level Political Forum – HLPF), ambalo pamoja na mambo mengine linashughulikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Mkutano huo ulifanyika mjini New York, Marekani kuanzia tarehe 9 – 18 Julai, 2019.

Mkutano huo ambao ulifanyika chini ya usimamizi wa Baraza la Masuala ya Uchumi na Kijamii la Umoja wa Mataifa (ECOSOC) ulikuwa na kaulimbiu inayosomeka **Kuwezesha watu na kuhakikisha ushirikishwaji (ujumuishi) na usawa** (Empowering People and Ensuring Inclusiveness and equality).

Mkutano wa mwaka 2019 ulipitia Malengo 6 ambayo ni Lengo Na. 4 - Elimu Bora; Na. 8 - Ajira za Staha na Ukuaji wa Uchumi na Na. 10 - Kupunguza Tofauti.

Malengo mengine ni lengo Na. 13 - Kuchukua Hatua Dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi; Na. 16 - Amani, Haki, na Taasisi Madhubuti na Na. 17 Ushirikiano ili kufanikisha Malengo.

Taarifa ya Tanzania ya kwanza ya Hiari (VNRs) kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu iliyoishirikisha sekta ya Elimu imekuwa ni kati ya taarifa nzuri zilizokidhi vigezo, na nchi nyingi zimetoa pongezi kwa kazi kubwa iliyofanyika ya maandalizi kitaifa na uliowashirikisha watendaji kutoka Tanzania bara na Zanzibar.

Madhumuni ya kuwasilisha taarifa hiyo ni kutoa taarifa za tathmini na hali halisi ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa nchi zilizotajwa kwa muda husika ili kufahamu mafanikio, changamoto na namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, ripoti hiyo ilikuwa na lengo la kuainisha vipaumbele kwa siku zijazo ili hatimae nchi ziweze kufikia malengo hayo ifikapo mwaka 2030. Pamoja na mkutano huo mkubwa, kulikuweko pia mikutano ya pembeni (side events) kuhusu mada mbalimbali zinazohusiana na utekelezaji wa Ajenda 2030.



Ujumbe kutoka Zanzibar ukiongozwa na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Ndugu. Mwita M. Mwita wakiwa Mjini New York kushiriki uwasilishaji wa Ripoti ya Hiari ya Tanzania

**UWAKILISHI WA ZANZIBAR KWENYE MKUTANO WA 2019**

Ujumbe wa Zanzibar kwenye mkutano huo uliongozwa na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Ndugu Mwita Mgeni Mwita, Kamishna wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini Ndugu Mashavu Khamis Omar ambae pia ni Mratibu na Msimamizi wa kuandaa ripoti kwa upande wa Zanzibar, Mtakwimu Mkuu wa Serikali Ndugu Mayasa Mahfoudh Mwinyi. Kutoka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto washiriki walikuwa ni Mkurugenzi wa Mipango Sera na Utafiti Ndugu Mhaza Gharib Juma na Mkurugenzi wa Ajira Ndugu Ali Ameir pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini Kitaifa ambae pia ni mjumbe wa timu ya Uratibu Kitaifa ya Uandishi wa Ripoti za Malengo ya kimataifa Ndugu Jamila Abbas Seif

Miongoni mwa maoni na mapendekezo ya jumla ya wadau yaliyotolewa kuhusiana na ripoti za elimu zilizowasilishwa ni pamoja na kuweko kwa matokeo yasiyoridhisha miongoni mwa watoto hasa katika maeneo ya kusoma na kuhesabu. Hata hivyo, ingawa kumekuwa na jitihada za wazi zinazoonekana katika kuongeza idadi ya uandikishwaji wanafunzi katika nchi zilizoko Kusini mwa jangwa la Sahara.

Vile vile kikao kilisisitiza haja ya kuwepo kwa usawa wa kijinsia katika uandikishaji wa watoto. Mambo mengine yaliyopendekezwa ni kufikia lengo la kuwa na Elimu bora kwenye sekta ya elimu na sio suala la mageuzi tena kama ilivyokuwa kabla. Hivyo mpango wa kubadilisha mawazo ya watu kifikra ili kufikia lengo lililokusudiwa ndio msingi katika utekelezaji wa dhamira hii ikiwemo kuwa na elimu shirikishi katika maeneo yote.



Wawakilishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango wakiwa kwenye Ofisi za Ubalozi Mjini New York wakijiandaa na matayarisho ya mwisho kabla ya kuwasilisha Ripoti ya Hiari

# UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU ZANZIBAR (SDGs)

**UTANGULIZI:**

Tathmini kadhaa zimekwishafanyika za Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya visiwa vya Unguja na Pemba kupitia utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa kupunguza Umasikini, MKUZA I, II na kwa kipindi hiki Utekelezaji wa MKUZA III ambapo utekelezaji wake unategemewa kukamilika sambamba na ukamilishaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020. Utekelezaji wa Malengo ya Milenia ulikwenda sambamba na Mpango wa kwanza wa kupunguza Umasikini, MKUZA I na II malengo yaliyotekelezwa kwa kipindi cha miaka 15 kutoka mwaka 2000 hadi mwaka 2015.

Malengo ya Milenia yapo manane (8) nayo ni Kutokomeza Umasikini, Kuimarisha elimu ya msingi, Kuwepo kwa usawa wa kijinsia, Kupunguza vifo vya watoto walio na umri wa mwaka 1 na miaka 5, Kuimarisha Huduma za Uzazi wa mama na watoto, Kupambana na maradhi ya Ukimwi, Malaria, TB n.k, Kuwepo Uhimili wa Mazingira na Kuimarisha Mashirikiano kwa ajili ya Maendeleo.

Baada ya kukamilika kwa Utekelezaji wa Malengo ya Milenia, dunia imekuja na mwelekeo mwengine wa Utekelezaji ambapo ni Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Malengo haya yapo 17. Utekelezaji wa Malengo hayo ya kidunia umeanza tokea mwaka 2016 na yanategemewa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka 15 hadi mwaka 2030. Utekelezaji wa MKUZA III unaendana sambamba na utekelezaji wa Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa SDGs.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Mwakilishi wa Shirika la UNESCO Tanzania Bw.Tirso Dos Santos



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Mwakilishi wa UNFPA nchini Tanzania Ms.Jacqueline Mahon

## LENGO 4

## ELIMU BORA


Ripoti iliyowasilishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeelezea kwa kina utekelezaji wa malengo sita (6) yaliyoainishwa kwa mwaka 2019. Kwa upande wa lengo la nne (4) la kuwa na Elimu bora, ripoti imeelezea maeneo tofauti ambapo kwa upande wa Zanzibar maeneo yafuatayo yalielezewa:

- Uandikishaji wa wanafunzi wa skuli za maandalizi (preprimary) umeongezeka kwa asilimia 20 kutoka wanafunzi 62,720 mwaka 2017 hadi wanafunzi 72,151 mwaka 2018. Kwa upande wa skuli za msingi uandikishaji umeongezeka kutoka wanafunzi 256,048 mwaka 2017 hadi wanafunzi 276,858 mwaka 2018, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.

- Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali Zanzibar inaufanyia tathmini mfumo wa mitihani kwa lengo la kuongezea ubora na uwe na wigo mpana zaidi kuliko ulivyo hivi sasa.

- Watu wasio na elimu kiujumla wameelezewa kufikia asilimia 16.3 ambapo mijini wapo asilimia 7.7 na vijijini wapo asilimia 23.9. Asilimia 11.7 ni wanaume na asilimia 20.6 ni wanawake.

- Kiwango cha ufaulu wa mitihani ya kidatu cha pili katika kipindi chote cha miaka minne (4) kwa wanafunzi wa kike, uko juu ukilinganisha na wanafunzi wa kiume. Kwa ufaulu wa kidatu cha nne wanafunzi wa kike na kiume wamelingana kuna utofauti kwa wanafunzi wa kiume kuzidi kidogo.Kwa upande wa kidatu cha sita, wanafunzi wa kike ufaulu wao upo juu kwa takriban ya miaka mitatu na mwaka mmoja tu wanafunzi wa kiume waliongoza kwa kiwango kidogo tu.



Elimu ya Sayansi


Wanafunzi wa Skuli ya Kwarara


Elimu ya Sayansi

LENGO 8

## KAZI ZENYE STAHA NA UKUAJI WA UCHUMI




Kwa mujibu wa Jarida ya Kiuchumi la mwaka 2018, kumekuwa na ongezeko la ukuaji wa uchumi kwa asilimia 7.1 kwa mwaka 2018 ukilinganisha na ongezeko la asilima 7.5. kwa mwaka 2017. Ongezeko hili limetokana na kuimarika sekta tofauti ikiwemo sekta ya utalii, biashara, kilimo na sekta nyengine, ambazo takwimu zinaonesha kuwa sio tu zimekuwa zikifanya vizuri katika miaka ya karibuni, lakini vile vile zimekuwa zikitoa fursa za kazi zenye staha na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa.

- Kumekuwa na ongezeko la watalii nchini kutoka watalii 433,474 mwaka 2017 hadi kufikia watalii 520,809 mwaka 2018
- Katika kipindi cha miaka mitano (2014-2018), uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.6. Kukua kwa juu kulionekana mwaka 2017 ambapo uchumi ulikuwa na kufikia asilimia 7.7.
- Kwa mwaka wa fedha 2015/16 makusanyo ya mapato yalikuwa TZS. bilioni 428.4 na kuongezeka kwa mwaka 2017/18 na kufikia TZS. bilioni 688.2.
- Usafirishaji wa bidhaa ulifikia thamani ya TZS. milioni 145,756.8 ambayo ni makubwa kwa asilimia 51.5 kwa kulinganishwa na mapato yaliyorikodiwa kwa mwaka 2016 ambayo yalifikia TZS. milioni 96,234.9.
- Thamani ya bidhaa zilizoingizwa ndani ya nchi zilifikia TZS. milioni 211,413.2 kwa mwaka 2017 ambapo kumekuwa na ongezeko la asilimia 26.5 ukilinganisha na TZS. milioni 167,088.0 zilizorikodiwa kwa mwaka 2016.


Sehemu ya Kazi za Staha Visiwani Zanzibar


Sehemu ya Kazi za Staha Visiwani Zanzibar


Sekta ya Utalii Zanzibar


Zao la Karafuu ni Sehemu ya Uchumi wa Zanzibar


Uchuuzi wa Samaki Zanzibar

## LENGO 10

## KUWA NA USAWA

Kupunguza utofauti kati ya mtu na mtu na nchi na nchi ni jambo ambalo limekuwa likisisitizwa sana na wataalamu wa masala ya uchumi duniani. Kiujumla upatikanaji wa usawa kupitia nyanja zote ulianzishwa mapema ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea yalipoasisiwa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Upatikanaji wa huduma za Elimu, Afya bila ya malipo kwa wananchi wote sambamba na kupiga vita matabaka miongoni mwa jamii, kunathibitisha dhamira ya Serikali katika kuleta usawa ndani ya jamii. Utekelezaji wa mambo yafuatayo unathibitisha zaidi jitihada za Serikali katika kuondosha utofauti miongoni mwa wanajamii.

- Elimu na Matibabu ni bure kwa wananchi wote
- Pencheni Jamii kwa wazee wote waliofikia umri wa miaka 70
- Mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya juu
- Ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima na huduma za matrekta
- Makaazi maalum kwa ajili ya wazee na watoto wanaoishi katika mazingira magumu



Elimu kwa Wenye Mahitaji Maalum


Huduma ya Pencheni jamii kwa Wazee

**LENGO**

**13**

## KUPAMBANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Zanzibar kama vilivyo visiwa vingine katika mwambao wa bahari ya Hindi na duniani kote, imekuwa muathirika mkubwa wa mabadiliko ya tabianchi kwa miaka kadhaa sasa. Visiwa vya Unguja na Pemba vimekuwa vikiathirika kutokana na kuongezeka kwa joto, upepo wenye kuvuma kwa kasi, ukame na mafuriko, mambo ambayo yamekuwa na athari ya moja kwa moja kiuchumi, kijamii na katika maendeleo.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imechukua hatua kadhaa zikiwemo zifuatazo:-

- Kufanya utafiti utakaobainisha athari za mabadiliko ya tabianchi kiuchumi.
- Kuzindua sera mpya ya Mazingira Zanzibar mwaka 1992.
- Kupitisha sheria mpya ya Mazingira Zanzibar ya mwaka 2015
- Kuunda Kamati Tendaji ya mabadiliko ya tabianchi ambayo wajumbe wake ni makatibu wakuu na wakurugenzi kutoka Wizara na Idara zote za Serikali ambazo kwa njia moja au nyengine zinahusiana na masuala ya tabianchi.
- Kuunda Kamati 45 za wanajamii Unguja na Pemba kwa lengo la kuhifadhi maliasili hasa misitu ambayo imeonekana kupotea kwa kasi kubwa kutokana na wanajamii kuitumia kama njia yao kuu ya kujipatia mapato.



Pwani ya Kizingo



Ukuta wa Forodhani



Pwani ya Kizingo

LENGO 16

## AMANI, HAKI, USAWA NA TAASISI ZA KIDEMOKRASIA




Shughuli kadhaa zimetekelezwa kupitia utekelezaji wa sharia zilizomo ndani ya lengo hili ambalo linazungumzia Amani, Haki na Taasisi Madhubuti za Kidemokrasia zikiwemo utetezi wa haki za watoto. Shughuli hizo ni pamoja na:-

- Ujenzi wa kituo cha utetezi wa watoto kinachojengwa huko Mahonda.
- Uwepo wa Sheria ya Kadhi
- Uimarishwaji wa Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka

Shughuli nyengine katika lengo hili ni pamoja na uokoaji wa watu kutokana na maafa ya aina tofauti yaliyotokea nchini ambao unafanywa bila ya ubaguzi kila inapotokea haja au ulazima wa huduma hiyo. Wananchi waliopatwa na mafuriko na kuokolewa mwaka 2015 walifikia asilimia 98 kwa mwaka ambapo lengo ni kuokoa asilimia 100 kwa mwaka 2020 ya waathirika.



Uzinduzi wa Mahakama ya Chake chake Pemba



Ofisi za Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar

LENGO 17

# USHIRIKIANO KATIKA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Mratibu Mkaazi wa Umoja wa Mataifa Nchini Tanzania Bw. Alvaro Rodrigues alipofika Ikulu Mjini Zanzibar kwa ajili ya kumuaga Rais baada ya kumaliza muda wake wa kazi nchini, tarehe 20 Agosti, 2019

Lengo hili limelenga katika kuimarisha mfumo wa utekelezaji wa malengo na kufufua ushirikiano wa kimataifa katika kuleta maendeleo.

Wakuu wa nchi na wawakilishi wa Mashirika na Jumuiya mbali mbali za kimataifa wamekuwa wakikutana na viongozi wakuu wa nchi kuzungumzia namna ya kuimarisha uhusiano baina ya pande husika na vile vile kushauriana kuhusu miradi ambayo inaweza kutekelezwa kwa pamoja baina ya pande hizo.

Mafanikio ya mikutano hiyo ni kuanzishwa kwa miradi kadhaa ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwa pamoja baina ya serikali na washirika wa maendeleo.

Kwa mwaka 2018/19 Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar umelenga kutekeleza jumla ya programu 27 na miradi 55 (miradi 14 mipya) yenye jumla ya TZS. bilioni 613 ikiwa ni ongezeko la TZS. bilioni 116.4 sawa na asilimia 23.4 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo ya mwaka 2017/18 ya TZS. bilioni 496.6.

Katika fedha hizo, jumla ya TZS. bilioni 464.2 sawa na asilimia 75.7 zimepangwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS. bilioni 75.6 ni ruzuku na TZS. bilioni 388.6 ni mikopo. Fedha hizo ni ongezeko la TZS. bilioni 83.71 sawa na asilimia 22, ikilinganishwa na makisio kwa mwaka 2017/18 ya jumla ya TZS. bilioni 380.5.

Miongoni mwa miradi mikubwa na midogo midogo iliyotekelezwa kupitia mpango huo ni pamoja na hii ifuatayo:-

- Ujenzi wa jengo jipya la abiria la uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III)
- Ujenzi wa ukuta wa bahari ya Mizingani
- Mradi wa ujenzi wa soko na kituo cha magari ya abiria Wete, Pemba;
- Mradi wa taa za barabarani
- Ujenzi wa viwanja vya michezo vya Mao Tse Tung
- Ujenzi wa soko la samaki Malindi
- Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Cheju, Bumbwisudi na Mwera
- Mradi wa ujenzi wa barabara za Bububu-Mahonda-Mkokotoni
- Ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja
- Uimarishaji wa maeneo ya kihistoria kwa kuyarejeshea haiba yake na kuwa na muonekano kama ulivyokuwa awali
- Mradi wa ujenzi wa skuli tisa za ghorofa za sekondari






# MALENGO 17 YA MAENDELEO ENDELEVU (SDGs)